Ndoto na Maono

Alhamisi, Mei 08, 2017

Utakatifu kwa Muumba Milele!

Ndoto na Maono

na

Jeanine SAUTRON
KANISA LA FILADELFIA,
"MASALIO",
wanaozitunza AMRI za MUNGU, pamoja na SABATO YA SIKU YA SABA, JUMAMOSI,
Na IMANI ya YESU.

IMANI ya YESU:

ROHO YA

UNABII.

(1) **UNABII WA GESI YA SARIN**(aina ya sumu inayotumika katika silaha za kemikali) **GESI YA MUSTARD-**(sumu ya mvuke(iliyotumika katika vita kuu ya kwanza) **UMEFUNULIWA NA YESU, MWANA WA MUNGU KATIKA BARAGUMU YA SITA YA UFUNUO. HAKUNA ATAKAYEOKOKA!**

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 1

MAONO

(2) Baada ya makaa kutupwa juu ya dunia, YESU alinifunulia: **"Baragumu ya sita ni mjapo wa kuogofya zaidi kuliko makaa yanayowaka moto."**

(3) Unabii huu umefunuliwa tu hivi punde na YESU, mwana wa Mungu.

(4) **Baragumu (tarumbeta) ya sita (6) iliyofunuliwa na YESU** katika *Ndoto na Maono* **itaua wakazi wa dunia bilioni mbili.** Theluthi moja ya wakazi watakufa kwa baragumu (tarumbeta) ya sita (6).

MAONO

(5) Katika maono haya, niliona farasi na wapanda farasi wao katika silaha za kivita za moto; na **moto, kiberiti**, na **moshi** ulitoka vinywani mwao. Wako njiani mwao, na jeshi hili litachukua juma moja(1) kuwasili duniani. **Katika baragumu hii ya sita, mapigo mawili(2) yanaenda kuwapiga wakazi wa dunia:**
Gesi ya **SARIN** na gesi ya **MUSTARD(HARADALI)**.

(6) YESU, mwana wa Mungu, aliniambia:

"Gesi hii ya SARIN na

gesi ya **Mustard zitakuwa kama nyuklia."**

(7) **"Gesi hizi za SARIN na Mustard zitakuwa na uwezo kama nyuklia. Ziko tayari:**

Hakuna atakayeokoka!"

(8) **"Silaha hizi ziko tayari. Wakazi bilioni mbili(2) watakufa kwa silaha hizi (kwa saratani za kila aina za mzio (allergy) hali ya ugonjwa inayompata mtu anapokula, gusa, nusa kitu fulani."**

(9) **"Tauni ya maiti za binadamu itaenda juu angani!"**

MAONO

(10) Niliona hili jeshi lililokuwa likiteremka duniani na farasi wanne (4) walikuwa mbele yao; mwekundu, mweupe, mweusi, na wa kijani kibichi, pamoja na wapanda farasi wao wepesi waliovaa silaha za moto, ndio waliofungua njia ya kuingia kwa jeshi hili.

(11) Nilikuwa katika maono. Niliona YESU ameketi juu ya kiti cha enzi, na malaika saba(7); na malaika wa sita aliinua sauti ya baragumu. Sauti hii ilikuwa ya huzuni, sauti ya mauti. Malaika walilia.

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 2

MAONO

(1) Sasa jeshi hili limetoka mbinguni. Walikuwa farasi wengi sana na wingi sana wa farasi wakiwa pamoja na wapanda farasi wao. Nao waliwasili duniani kwa kazi yao ya mauti.

(2) YESU alinifunulia, **"Baragumu ya sita (6) inatisha zaidi kuliko maji yanayoinuka, mito inayovunja kingo zake, n.k. katika nchi; baragumu ya sita (6) inatisha zaidi."—**Nilitetemeka.

(3) YESU alifunua: "**Ni pigo lisilo na harufu, la kimya. Bilioni mbili(2) ya wakazi watakufa kwa haya mapigo mawili."**

(4) YESU amenifunulia, na bado anavuta usikivu wangu kwa hilo: **"Wala si kwa silaha nzito, wala mizinga, wala kwa maaskari au nyuklia. Ni silaha mbili za uwezo, za siri, silaha zisizoonekana zitakazowashangaza wakazi wa dunia. Hazina harufu."**

(5) Uropa haitaachwa. Watu wadhaifu, kama watoto, watakufa kutokana na **allergies (hali ya kuadhirika vibaya au kuugua unapokula au kunusa au kuguza kitu fulani). Matunda na mboga zitakuwa na sumu**; na maumbile yote, wanyama wa mbugani na wa misituni wataadhirika na mapigo haya.

(6) Kwa kadiri mashamba ya mboga yasiolimwa kwa kutumia kemikali yanavyohusika, mboga zote zitakuwa za sumu.

(7) YESU aliniambia: "**Mapigo haya ni kwa sababu ya midomo ya farasi**. **Moto, kiberiti, na moshi unatoka vinywani mwao. Hakuna kilicho na uhai (kutotumia kemikali) kwa wakati huu. Kila kitu kina sumu."**

(8) YESU mwenyewe alikuja na kuniambia kuwa shamba langu lina sumu kwa sababu ya baragumu ya sita(6).

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 3
MAONO

(1) Mbinguni niliona kuwa kiti cha enzi kikubwa cheupe kilisimamishwa. YESU mwana wa Mungu, alikuja akaketi juu ya hiki kiti cha enzi. Maneno haya yaliandikwa juu ya vazi lake.

MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA.

(2) Malaika saba (7) walikuja wakajiweka karibu sana na kiti cha enzi; na YESU aliamrisha malaika wa sita(6) apige baragumu.

(3) Katika maono haya, usikivu wangu ulivutwa kwa malaika wa sita(6). YESU alimfanya aje karibu na kiti chake cha enzi, akampatia kazi ya kwenda kwa mto Frati, kwenda kule na kuwafungua wale malaika wanne waliofungwa kwa mto huu. Aliondoka, nami sikumwona malaika huyu.

(4) Wakati alipokuwa hayuko, niliona farasi wanne(4), wakiwa pamoja na wapanda farasi wao, wakija mbele ya kiti hake cha enzi:

farasi mweusi
farasi mwekundu
farasi wa kijani kibichi, na
farasi wa kijivujivu.

(5) Yeye (YESU) alizungumza na wapanda farasi hawa. Baada ya maongezi haya, walichukua nafasi zao mbele ya jeshi la mbinguni.

(6) Niliona kuwa hili jeshi lililokuwa linasubiri agizo la kuondoka, nami niliona malaika, aliye malaika wa sita(6) akiwasili. Alichukua tena baragumu yake na kumwambia YESU: "Wale malaika wanne (4) walio katika mto Frati wamefunguliwa. Nimetimiza kazi yangu maalumu."

(7) Alizungumza kwa muda mfupi na YESU, ambaye alimwambia arudi katika nafasi yake pamoja na wale malaika wengine walio na baragumu.

MAONO

(8) Niliona kuwa jeshi hili limewasili duniani. Katika maono haya YESU alikuwako. Alipokea jeshi hili. Aliponiona, aliniambia:

"Neema yangu inakutosha."

(9) Niliona jeshi hili likisimama juu ya ardhi. Agizo lilitolewa la kuwatenga kwa makundi mawili (2) ya wengi sana.

(10) Walipowasili tu duniani, nilitambua kuwa mikia ya farasi ilitengenezwa kwa nyoka wadogo wasiohesabika waliokuwa wakisonga kwa kujisokota sokota. Nilifadhaika, niliogopa sana.

(11) YESU aliniambia: **"Usiogope; hawatakufanyia madhara yoyote. Neema yangu inakutosha wewe."**

(12) Farasi wamethibitiwa juu ya dunia. Jeshi hili lilisimama YESU alipotoa agizo. Aliniambia, **"Tazama!"**

(13) Nilisisimka kwa hofu katika kuangalia mikia ya farasi hawa. Nikiwa nimefadhaika, niliona nyoka wadogo wasiohesabika ambao walitengeneza mikia ya farasi hawa.

(14) Nilipokuwa nikiangalia, nilitambua kuwa juu ya mikia yao nambari ya kweli (lakini isiyo bayana) ya tarakimu tatu: **666**, zilizoonekana juu ya nuru yenye kurudisha mwanga wa samawati nyepesi uliotoka sehemu ya nyuma ya kila farasi.

(15) Jeshi hili lilipokuwa mbinguni, sikuweza kuona nambari **666**, yoyote.

(16) Nikiwa nimeshindwa na nyoka na nambari hii: **666,** niliona katika maono kwamba nambari ya simu za rununu zilitiwa sumaku kwa nyoka zile, ambazo ni mikia ya farasi, nazo hazikuwa zikianguka chini. Vitu vilining'inizwa kwa nguvu, vimetiwa sumaku kwa wale nyoka. Kila kifaa cha kubebeka kiliunganishwa kwa nyoka kupitia nambari yake: **666.**

MAONO

(17) Ajabu, nilipokuwa karibu na mkia wa farasi, niliona kuwa nyoka wale, waliotiwa sumaku kwa vitu hivi, walipeana uhai kwa simu hizi za rununu zilizofanya kazi kana kwamba nyoka wa hao farasi walikuwa wamilikaji na watumiaji wa hizo.

(18) Niliona nambari **666** imeonyeshwa kwa herufi kubwa juu ya hizi simu za rununu. Mikia ya nyoka ilitiwa sumaku kwa simu za seli zote duniani. Ajabu, tena, niliona sanamu za kweli (zisizo bayana, sanamu za picha, zilizonakshiwa(chorwa) juu ya sikrini zilizokuwa zikitumika kikamilifu.

MAONO

(19) Katika maono haya, nilimwona YESU, alikuwa na jeshi lake duniani. Alizichukua simu za seli, akiziondoa moja baada ya ingine, akizivuta, ili kuzitenganisha kutoka kwa mwili wa nyoka zile. Kisha akaziponda chini ya miguu yake akitamka ghafla kwa hasira:

"Mauti! Mauti! Mauti!"

(20) Nilijua maana ya neno hili katika lugha ya *Kifaransa:*

"La mort! La mort! La mort!"

(21) Nilikuwa na wasiwasi. YESU alinitazama na kuniambia,

“Neema yangu inakutosha.
Hakuna atakayeokoka!”

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 4

MAONO

(1) **Alama 666**
ya mnyama
iko lakini
haionekani kwa
macho na haigusiki.

(2) Niliona katika maono haya watumiaji wa simu hizi za rununu zilizo na hesabu **666,** zilizojidhihirisha katika vipaji vya nyuso za wanaozitumia, za wenye simu.

(3) Hesabu **666** ilirudisha nuru ya mfano wake ju ya vipaji vya nyuso zao, kama picha iliyoko lakini isiyo halisi, tarakimu hizi tatu: **666**, katika rangi ya samawati nyepesi iliyo mahali pa nyuma ambayo hung’aa usiku.

(4) Kipaji cha uso na mkono wa kuume ndizo zilizoshikilia tarakimu hizi tatu(3). Ilikuwa ya kuogofya! **Watumiaji wa vitu hivi walichukua juu yao, juu ya miili yao, hesabu 666, hesabu ya mnyama, shetani.**

(5) Maono yanaonyesha kwamba **kila mtumiaji wa simu hizi za mkononi alikuwa na nyoka aliyeunganishwa na ubongo wake na chombo chake cha mkononi,** ambacho kwa hicho **angeweza kununua na kuuza.**

(6) Wale wote waliokuwa na **simu za kiseriti cha mguso** walipokea:
chapa,
alama ya shetani,
hesabu **666**,
chapa iliyoko ila isiyo bayana.

MAONO

(7) Niliona kwamba walikuwa ni nyoka katika baragumu ya sita waliopeana uhai kwa simu za rununu kupitia kwa hesabu ya mnyama 666, nyoka katika baragumu ya sita(6).[1]

(8) Alama 666 ya mnyama katika kipaji cha uso haijafunikwa utando mwilini. Alama hii 666 ipo ila sio bayana. Kupokea alama ni kupokea hesabu hii 666, ambayo ni alama isiyo bayana katika kipaji cha uso. Alama hii inakuwa hai kupitia hesabu: **666.**

(9) Picha hii ya virtual(iliyopo ila haionekani) husonga kwa kufuata mwienendo yote ya mwenye simu hiyo. Picha hii haimwachi. Iko katika kipaji cha uso na katika mkono wa kuume. Hii ni alama ya mnyama.

(10) Wakati wa mchana, picha hii **666** ya virtual(isiyo bayana) ni nyeusi sana, na jioni inarudisha nuru ya fluorescent(yenye kuakishi (rudisha) mwanga), katika tarakimu 666 nyeupe, ili kwamba malaika waweze kuwaona watoto wa ibilisi.

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 5

MAONO

(2) **Pikseli inaonekana.**
kadi ya benki inaonekana.
Simu ya mkononi
inaonekana.

kwa vile vitu hivi vinaweza kuguswa, kushikwa. Ni kwamba viko na alama ya mnyama **666**.

(2) Alama haionekan; kama uko na vitu hivi; kadi, RFID, *simu ya mkononi*, kadi ya benki, hizi zinakupa haki ya kupokea **alama ya VIRTUAL**(inayoonekana kuwa halisi ila sio bayana) juu ya kipaji cha uso na katika mkono wa kuume ili ununue na kuuza.

---

1 [13]Malaika wa sita akapiga baragumu. Nikasikia sauti iliyotoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyo mbele za Mungu. [14]Ikimwambia yule **malaika wa sita aliyekuwa na baragumu moja,** “Wafungue hao malaika wanne waliofungwa kwenye mto mkubwa Frati. [15]Wale malaika wanne wakafunguliwa, waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka, ili **kwamba waue theluthi moja ya wanadamu**. [16]Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa **milioni mia mbili**. Nilisikia hesabu yao. [17]Hivyo ndivyo nilivyowaona hao farasi katika maono, na wale walioketi juu yao, wakiwa na dirii kifuani, kama za moto mwekundu na za samawi, na za kiberiti cha manjano; **na vichwa vya simba. Katika vinywa vyao hutoka moto, moshi, na kiberiti.** *Ufunuo* 9:13-17.

[12]Na huyo wa sita aliimimina bakuli yake juu ya **mto mkubwa Frati**. Maji yake yakakauka, ili njia itengenezwe kwa **wafalme** watokao katika maawio ya jua. [13]Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. [14]Maana hizo ni **roho za mashetani, zifanyazo ishara; zinazowaendea wafalme wa ulimwengu wote unaokaliwa na watu, ili kuwakusanya pamoja kwa vita** vya siku ile kuu ya Mungu, mwenyezi. [15]“**Tazama, naja kama mwivi**. Heri akeshaye na kuyatunza mavazi yake, ili asiende uchi, hata wakaiona aibu yake.” [16]Akawakusanya pamoja mahali paitwapo kwa Kiebrania Megiddo [*Harmagedoni*] *Ufunuo* 16:12-16.

(3) Ni nyoka katika baragumu ya sita(6) ambao huvipa uhai *vitu hivi vya kuchukulika*; RFID, microchip na kadi zote za benki, vikiruhusu watu kununua na kuuza. Unapokea alama ya virtual ya 666 ya mnyama, maana vitu hivi vina alama **666** ya shetani iliyounganishwa na nyoka za baragumu ya sita(6) zinazoviletea uhai.

(4) YESU alisema:

"Kifo! Kifo! Kifo!"

(5) **"Utakufa kwa kuiuza roho yako kwa shetani, na kwa sababu ya kupokea alama yake virtual**(inayoonekana kuwa halisi ila sio bayana) **katika kipaji cha uso wako na katika mkono wako kwa kutumia aidha RFID, au chombo cha kuchukulika mkononi(simu), au kadi ya benki."**

(6) **"Theluthi moja ya wakazi watakufa kwa nyoka walio na alama ya mnyama 666. Hawataokoka!"** YESU alisema.

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 6

(1) **Ujumbe unaohusu baragumu ya sita(6) umetolewa duniani**. Unabii huu uko njiani.

(2)YESU alikuja na kunifunulia **siku, tarehe** na **saa. Uliondoka tayari!**

(3) Unabii huu ulitukia
mwezi wa **Agosti 26**
saa **mbili jioni (8:00pm)**
mwaka wa **2016.**

(4) Ni kuanzia tarehe hiyo ya unabii huu kwamba hakuna tena *chakula* chenye uhai. **Vyote vimekuwa sumu.**

(5) Watoto kule Uropa watakufa kutokana na miwasho inayotoka katika vinywa vya farasi: **moto, kiberiti**; na **moshi**, uliofunuliwa na YESU katika unabii huu wa kutisha wa baragumu ya sita(6).

(6)YESU alifunua: "Sio **kwa silaha nzito za jeshi la dunia, wala kwa mizinga mikubwa, wala kwa nyuklia, silaha mbili za kutisha. Mapigo mawili ya kutisha yatawapiga wakazi wa dunia: Theluthi moja ya idadi ya watu wa dunia itatoweka kupitia gesi ya SARINI na gesi ya MUSTARD. Hakuna atakayeokoka!"**

(7) **"Silaha hizi ni:**
gesi ya SARIN, **na gesi ya MUSTARD**, **silaha mbili (2) za kutisha, zinazofanana na nyuklia."**

(8) "**Lakini Uropa haitaachwa**." YESU aliniambia, "**kutoka kwa ile gesi ya SARIN na gesi ya MUSTARD**, **moto, kiberiti na moshi, utokao katika vinywa vya farasi wale**."

(9) Unabii uliofunuliwa na YESU katika baragumu ya sita ni wa namna hii,

saa 8:00 pm
katika **mwezi wa Agosti, 2016.**
Ilikuwa **ni Ijumaa.**

(10) Baada ya ufunuo huu wa kutisha, sikuona tena maumbile katika uzuri wake. Yote imesimamishwa na ni chungu. Kila kitu kimebadilika kwangu pande zote.

(11) **Uropa haitaokoka!**

(12) "**Kusumisha huku**," YESU aliniambia, "**kutaathiri watoto, vijana wa kiume na wa kike zaidi. Kizazi hiki cha watu wa umri wa miaka 45 hakitapita hadi yote yaliyofunuliwa yatukie**."

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 7

(1) **Muhuri wa Mungu**

(2) **Muhuri wa Mungu sio virtual.**

(3) Nimeona kwamba muhuri wa Mungu ni mhuri katika kipaji cha uso wa aliyekombolewa. Mhuri huu una sahihi hii:

Mungu, Yerusalemu mpya."

(4) **Ni nanga ndani ya mwili.**

(5) Shetani na pepo zake hawawezi kuondoa nanga hii. Ni ya kimbingu.

Ndoto na Maono
Sura ya 532, Maono Namba 8

(1)Baada ya ufunuo huu wa baragumu ya sita(6), muda fulani ulipita. Nilipata maono mengine.

MAONO

(2) Niliona kwamba jeshi hili limerudi mbinguni likiwa katika hali ya kupumzika, na baada ya kupigana vita kuu na kukamilisha kusudi la Mungu duniani.

(3) Niliona malaika wenye nguvu walioitwa kwa amri ya YESU, ili kuondoa nyoka wale waliounda mikia ya farasi.

(4) Niliona wale nyoka hai, ambao walisonga kwa kujisokota sokota, walibanduliwa kutoka kwa farasi na kutupwa chini mchangani kwa nguvu. Ndipo hawa malaika waliwaponda chini ya miguu yao.

(5) Walikuwa wamalize kazi hii kabla ya SABATO waliniambia.

(6) Katika maono haya, malaika aliyehudumu aliniruhusu nikae ubavuni mwake, naye aliniambia, "Nakujua. Wewe ni Jeanine. YESU, Bwana wangu

alitaka akuone hapa ili akuonyeshe kuwa mbinguni hakuna uovu, wala alama ya mnyama, wala hesabu ya mnyama. YESU, Bwana wetu, alitaka ushuhudie kuharibiwa kwao. Nyoka hawa unaowaona juu ya farasi wote wataondolewa na kuuawa.”

(7) Niliona kwamba nyoka hawa waliharibiwa mbinguni. Malaika waliwaua wote; *wali*waponda chini ya muguu yao.

Jeanine Sautron